

Kuhusu ugonjwa wa coronavirus (COVID-19)

Vinaenea Vipi?



Virusi vya Covid-19 huenea kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Mtu aliyeambukizwa hudondosha matone ya mate anapopiga chafya, kukohoa, kuzungumza au hata kupumua tu. Watu waliokaribiana (chini ya mita 1-2) wanaweza kuambukizana virusi kupitia vinywa vyao, pua au macho. Virusi pia vinaweza kuambukiza ikiwa mtu atagusa kitu kilichochofuliwa (k.m nyundo, kishikio cha mlango), kisha kugusa uso wake.

Mtu aliyeambukizwa huanza kuonesha dalili siku 5-6 baada ya kuambukizwa, lakini inaweza kufika hadi siku 14. Watu wengine hawaoneshi dalili zozote.

Watu walioambukizwa, wanaambukiza Zaidi (wanaweza kuambukiza wengine) siku 2-3 kabla ya kuonesha dalili zozote, na pia siku 8 baada ya dalili kuanza kuonekana. Watu ambao kamwe hawaoneshi dalili zozote wanaweza pia kusambaza virusi, ingawa kuna uwezekano mdogo hali hii kutokana

Dalili ni zipi?

Virusi vya Corona vinaweza kuathiri viungo mbalimbali! Dalili kuu ni **homa, kikohozi na hubanwa pumzi.**

Dalili nyingine zinazo ripotiwa mara kwa mara ni pamoja na: **maumivu ya misuli, kupoteza ladha au harufu, maumivu kooni na/au mafua.**

Dalili zisizo za wazi Zaidi ni kuhara, kichefuchefu/kutapika, maumivu ya kichwa na kukabwa na mafua.

COVID-19 huathiri watu tofauti kwa namna tofauti. Baadhi yao kamwe hawaneshi dalili zozote, Wengi kati ya wanaougua huonesha dalili dhaifu; karibu aslimia 15 hupata maambukizo makali (k.m., kubanwa pumzi, nimonia) na aslimia 5 huwa na hali mbaya ambayo huweza kusababisha kifo (k.m. kushindwa kupumua au viungo kutofanya kazi)



HOMA



KUKOHOA



UPUNGUFU WA PUMZI

Nani yuko hatarini?

Wazee (Umri zaidi ya miaka 60) na watu wa umri wowote ambao kinga zao za mwili zimeathirika na/au hali mbaya ya kiafya (k.m., pumu, silicosis, ugonjwa wa sukari, shida za moyo na mishipa, ukimwi, unene kupita kiasi, uvutaji sigara, athari sugu za zebaki) wako kwenye hatari ya kupata maambukizo mazito ya covid-19 na shida za kimatibabu. Lakini watu wa umri wowote wanaweza kupatwa na maambukizi dhaifu au makali.

Simu ya dharura ya COVID-19:

Kumbuka kuwa ujuzi juu ya Covid-19 unatokea kila siku na mwongozo unaweza kubadilika.

Tafuta habari kutoka kwa mamlaka yako ya afya na ufuate sera za kitaifa.